# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

اياتها ٩٩ (١٥) سورة الحجر مكية (٥٤) ركوعاتها ٦

Ina Aya 99 | Ina Makaru 6

# SURATUL HIJR

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Alif Lam Ra. Hizi ni Aya za Kitabu kilichokusanya kila yanayohitajiwa na kikayadhihirisha kwa vizuri.

2. Mara nyingi wale waliokufuru watatamani (huko Motoni) lau wangalikuwa Waislamu.

3. Waache wale (chakula) na wafurahi na liwadanganye tumaini la uwongo (la kuwa wataghufiriwa). Karibuni hivi watajua (ya kuwa si kweli tumainio lao hilo).

4. Na hatukuuangamiza mji wowote ule ila ulikuwa na muda wake maalumu.

5. Hawawezi watu wowote kuitangulia ajali yao (muda wao), wala hawawezi kukawia (baada ya kufika muda wao).

6. Na walisema (kwa stihizai): "Ewe uliyeteremshiwa mauidha! Hakika wewe ni mwendawazimu."

7. "Mbona hutuletei (hao) Malaika (wa kutuangamiza) ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli?"

8. (Mwenyezi Mungu anawaambia). Sisi hatuteremshi Malaika ila kwa haki (wakati wa kuangamizwa kwao unapothubutu); na hapo hawatapewa muhula (ila wataangamizwa tu).

9. Hakika Sisi ndio tulioteremsha mauidha haya (hii Qurani); na hakika Sisi ndio tutakayoyalinda.

بسم الله الرحمن الرحيم

الٓرٰ تلك اٰيٰت الكتٰب وقراٰن مبين ①

ربما يود الذين كفروا لو كانوا مسلمين ②

ذرهم ياكلوا ويتمتعوا ويلههم الامل فسوف يعلمون ③

وما اهلكنا من قرية الا ولها كتاب معلوم ④

ما تسبق من امة اجلها وما يستاخرون ⑤

وقالوا يٰايها الذي نزل عليه الذكر انك لمجنون ⑥

لو ما تاتينا بالملٰئكة ان كنت من الصٰدقين ⑦

ما ننزل الملٰئكة الا بالحق وما كانوا اذا منظرين ⑧

انا نحن نزلنا الذكر وانا له لحٰفظون ⑨

---

2. Lakini kutamani kwao hakutakuwa na faida nao. Yaleyti Haileti.

3. Wanasemezwa wale ambao hima yao ni katika kula na kustarehe tu. Hima ya kinyama. Hima yako iwe ni kutengeneza dunia yako na ya wenzako na Akhera.

6-7. Namna walivyokuwa wanajitahidi kumpachika Mtume sifa asizokuwa nazo, na wana yakini kuwa Mtume hana sifa hizo. Wanavurumiza tu makusudi. Basi na sisi tukivurumiziwa tusione kitu. Tusishughulike na kuwajibu. Tushughulikie yenye faida. Mwislamu hapotezi wakati wake kwa jambo lisilokuwa na faida.

9. Maneno haya ya Qurani yatasalia maisha bila ya kupotea hata harufu moja. Na wowote watakaotaka kubadilisha harufu moja tu hii watafedheheka; itambulikane pale pale kuwa harufu hiyo SIYO; kama ilivyofanya safari hii Serikali ya Uyahudi (ya Israili); ilitabiisha Qurani ikabadilisha kidogo baadhi ya vijineno ikatangazwa ulimwenguni; papo hapo ilijulikana.

10. Na bila shaka tuliwaleta (Mitume) kabla yako katika makundi ya (watu) wa mbele huko.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي شِيَعِ الْأَوَّلِينَ ﴿١٠﴾

11. Na hakuwafikia Mtume yoyote ila walimfanyia stihizai.

وَمَا يَأْتِيهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿١١﴾

12. Na kama hivi tunaingiza (tabia hiyo ya stihizai), katika nyoyo za hawa maasi (wa umma wako)

كَذَٰلِكَ نَسْلُكُهُ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٢﴾

13. Hawayaamini haya, na hali ya kuwa imewapitia mifano ya watu wa mbele huko (wakaona namna walivyoangamizwa).

لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ وَقَدْ خَلَتْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣﴾

14. Na lau tungaliwafungulia (hao makafiri) mlango wa mbingu,* na wakawa wanapanda (na kushuka kama walivyotaka, ili uwe ndio muujiza wa Mtume)

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٤﴾

15. Basi wangalisema: "Macho yetu yamerogwa tu, bali sisi (nafsi zetu) ni watu tuliorogwa (tunaona kinyume cha mambo)."

لَقَالُوا إِنَّمَا سُكِّرَتْ أَبْصَارُنَا بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُورُونَ ﴿١٥﴾

16. Na hakika tumeweka katika mbingu, vituo (vya nyota) na tumezipamba (hizo mbingu) kwa ajili ya wale wanaozitazama

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَزَيَّنَّاهَا لِلنَّاظِرِينَ ﴿١٦﴾

17. Na tumezilinda na kila shetani ambaye hufukuzwa (kila anapotaka kuja kusikiliza yanayopita huko mbinguni)

وَحَفِظْنَاهَا مِن كُلِّ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿١٧﴾

18. Lakini asikilizaye kwa wizi, basi mara humfuata kijinga kilicho dhahiri.

إِلَّا مَنِ اسْتَرَقَ السَّمْعَ فَأَتْبَعَهُ شِهَابٌ مُّبِينٌ ﴿١٨﴾

19. Na ardhi tumeitandaza na humo tumeweka milima na tumeotesha kila kitu kwa kiasi (chake).

وَالْأَرْضَ مَدَدْنَاهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنبَتْنَا فِيهَا مِن كُلِّ شَيْءٍ مَّوْزُونٍ ﴿١٩﴾

20. Na tumekufanyieni humo vitu vya (kuendesha) maisha (yenu) na (vya maisha ya) wale ambao (mumewamiliki wala) nyinyi sio wenye kuwaruzuku. (Waruzukaji wa hakika ni sisi—Mwenyezi Mungu).

وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعَايِشَ وَمَن لَّسْتُمْ لَهُ بِرَازِقِينَ ﴿٢٠﴾

21. Na hakuna chochote ila asili yake inatokana na sisi; wala hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu (si ovyo ovyo tu).

وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا عِندَنَا خَزَائِنُهُ وَمَا نُنَزِّلُهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَّعْلُومٍ ﴿٢١﴾

---

Na maana yake pia yatasalia yale yale na haitabainika hata mara moja kuwa hivyo sivyo zinavyosema Ilimu za sasa. Qurani mpaka leo—na mpaka mwisho wa ulimwengu—haikusema kitu ambacho imebainika sasa kuwa sivyo hivyo zinavyosema Ilimu za Science na nyenginezo zote zilizo Ilimu za kweli. Amekwisha kusema Mwenyewe Mwenyezi Mungu kuwa Qurani 'Haiijii hii Qurani kukosa upande wo wote ule—mbele yake wala nyuma yake."

14-15. Katika inadi yao, hata wangepewa hiyo miujiza wanayoitaka, hata ya kupanda mbinguni; basi wangesema 'Ni kiini macho; tunajiona tu kuwa tunapanda mbinguni, wala hatupandi hivi. Tumekaa sisi, tunajiona tu kuwa tunapaa wala hatupai . . .' Binaadamu ni mshindani kweli kweli kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 54 ya *Suratul Kahf.*

19. Kila kitu Mwenyezi Mungu anakifanya kwa kiasi chake (kipimo chake) si ovyo tu.

وَأَرْسَلْنَا الرِّيٰحَ لَوٰقِحَ فَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَأَسْقَيْنٰكُمُوهُ وَمَآ أَنْتُمْ لَهُۥ بِخٰزِنِينَ ﴿٢٢﴾

22. Na tunazileta pepo zimejaa umande (wa kufanya mawingu) na tunateremsha maji (ya mvua) kutoka katika mawingu hayo(yanayochungwachungwa na hizo pepo pia), kisha tunakunywesheni maji hayo (na wanyama wenu na miti yenu na mengineyo). Wala si nyinyi muyawekao (katika ardhi yakawa mito, maziwa, mifereji, visima. . . .).

وَإِنَّا لَنَحْنُ نُحْيِۦ وَنُمِيتُ وَنَحْنُ الْوٰرِثُونَ ﴿٢٣﴾

23. Na sisi ndio tunaohuisha na tunaofisha; na sisi ndio warithi (wa yote haya wakati ambao hapana chochote kitakachokuwa kihai).

وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنْكُمْ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَـْٔخِرِينَ ﴿٢٤﴾

24. Na tunawajua watanguliao(waliokwishakufa) katika nyinyi, na tunawajua wachelewao (walio wahai na wasiokuja ulimwenguni bado).

ع وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَحْشُرُهُمْ إِنَّهُۥ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥﴾

25. Na bila shaka Mola wako, Yeye ndiye atakayewakusanya. Hakika Yeye ni Mwenye hikima na Ajuaye (kila jambo).

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسٰنَ مِنْ صَلْصٰلٍ مِنْ حَمَإٍ مَسْنُونٍ ﴿٢٦﴾

26. Na tulimuumba mwanaadamu kwa udongo mkavu unaotoa sauti (unapogongwa), unaotokana na matope meusi yaliyovunda.

وَالْجَآنَّ خَلَقْنٰهُ مِنْ قَبْلُ مِنْ نَارِ السَّمُومِ ﴿٢٧﴾

27. Na majini tuliwaumba kabla, kwa moto wa upepo wenye joto (kubwa kabisa).

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ إِنِّي خٰلِقٌۢ بَشَرًا مِنْ صَلْصٰلٍ مِنْ حَمَإٍ مَسْنُونٍ ﴿٢٨﴾

28. Na (kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika, "Hakika Mimi nitamuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda."

فَإِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُۥ سٰجِدِينَ ﴿٢٩﴾

29. "Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na Mimi, basi mumuangukie kwa kumtii."

فَسَجَدَ الْمَلٰٓئِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿٣٠﴾

30. Basi Malaika wakatii wote pamoja

إِلَّآ إِبْلِيسَ أَبَىٰٓ أَنْ يَكُونَ مَعَ السّٰجِدِينَ ﴿٣١﴾

31. Isipokuwa Iblisi; alikataa kuwa pamoja na waliotii.

قَالَ يٰٓإِبْلِيسُ مَا لَكَ أَلَّا تَكُونَ مَعَ السّٰجِدِينَ ﴿٣٢﴾

32. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Ewe Iblisi! Imekuwaje? Hukuwa pamoja na waliotii?"

قَالَ لَمْ أَكُنْ لِأَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهُۥ مِنْ صَلْصٰلٍ مِنْ حَمَإٍ مَسْنُونٍ ﴿٣٣﴾

33. Akasema "Siwezi kumtii mtu uliyemuumba kwa udongo mkavu unaotoa sauti, unaotokana na matope yaliyovunda."

قَالَ فَاخْرُجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَجِيمٌ ﴿٣٤﴾

34. Akasema (Mungu): "Basi toka humo, na hali ya kuwa wewe (sasa) ni mwenye kufukuzwa na kubaidishwa na rehema"

---

27. Katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 28 wanatia ukafiri wao ule wa kukataa Majini — ambao tumeutaja katika marejezo ya Aya ya 112 ya *Suratul An-am* — na wametia ukafiri wao pia ule wa kusema kuwa Nabii Adamu siye baba wa wanaadamu wote. Na tumeyarejeza haya katika marejezo ya Aya ya 30 ya *Suratul Baqarah*.

35. "Na kwa yakini itakuwa juu yako laana mpaka siku ya malipo."

وَإِنَّ عَلَيْكَ اللَّعْنَةَ إِلَىٰ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٣٥﴾

36. Akasema (Iblisi): "Mola wangu! Basi nipe nafasi (nisife) mpaka siku watakayofufuliwa (viumbe vyote)."

قَالَ رَبِّ فَأَنظِرْنِي إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿٣٦﴾

37. Akasema (Mungu): "Hakika wewe (nimekwisha kufanya) katika wale waliopewa nafasi "

قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنظَرِينَ ﴿٣٧﴾

38. "Mpaka siku ya wakati uliowekwa; (ukifika wakati huo utakufa)."

إِلَىٰ يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ ﴿٣٨﴾

39. Akasema: "Mola wangu! Kwa sababu umenihukumu kupotea, basi nitawapambia (viumbe vyako upotofu) (upotevu) katika ardhi na nitawapoteza wote."

قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَلَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾

40. "Isipokuwa wale waja wako waliosafika kweli kweli."

إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٤٠﴾

41. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Hii njia yao ya (kuja) kwangu imenyoka (wanaweza kunijia wakati watakao)."

قَالَ هَٰذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾

42. "Hakika waja wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao; isipokuwa wale wenye kukufuata (kwa khiari zao) katika hao wapotofu (wapotevu)."

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾

43. Na bila shaka Jahanamu ndipo mahali pao walipoahidiwa wote

وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٣﴾

44. Ina milango saba; na kwa kila mlango iko sehemu yao iliyogawanywa (ya kuwa hii ya mlango fulani na hii ya mlango fulani).

لَهَا سَبْعَةُ أَبْوَابٍ لِّكُلِّ بَابٍ مِّنْهُمْ جُزْءٌ مَّقْسُومٌ ﴿٤٤﴾

45. Na hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu watakuwa katika Mabustani na chemchemu (zinazopita mbele yao huko; waambiwe).

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٤٥﴾

46. "Yaingieni salama usalimini (kwa salama na muwe katika amani)."

ادْخُلُوهَا بِسَلَامٍ آمِنِينَ ﴿٤٦﴾

47. Na tutaondoa mifundo iliyokuwa vifuani mwao, na (watakuwa) ndugu (wenye kupendana) (waliokaa) juu ya viti vya kifalme, wameelekeana (wanazungumza kwa furaha kubwa).

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِم مِّنْ غِلٍّ إِخْوَانًا عَلَىٰ سُرُرٍ مُّتَقَابِلِينَ ﴿٤٧﴾

48. Haitawagusa humo taabu wala pia humo hawatatolewa.

لَا يَمَسُّهُمْ فِيهَا نَصَبٌ وَمَا هُم مِّنْهَا بِمُخْرَجِينَ ﴿٤٨﴾

---

39. Tumeisema kwa urefu—katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am*—habari ya kuongolewa na ya kuachiwa kupotea.

47. Watu wakiwa Peponi hawatakumbuka ugomvi wao wa kila namna waliokuwa nao duniani na mifundo yao. Wote wanapendana pasina mfano — Raha mustarehe.

49. Waambie waja wangu ya kwamba Mimi ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu

نَبِّئْ عِبَادِيٓ أَنِّيٓ أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٤٩﴾

50. Na hakika adhabu Yangu ni adhabu inayoumiza kweli kweli.

وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿٥٠﴾

51. Na uwaambie khabari za wageni wa (Nabii) Ibrahimu.

وَنَبِّئْهُمْ عَنْ ضَيْفِ إِبْرٰهِيمَ ﴿٥١﴾

52. Walipoingia kwake na wakasema: "Salaam" (Salaamun Alaykum. Akawajibu; kisha) Akasema (alipoona wamekataa kula chakula alichowaekea); "Kwa hakika sisi tunakuogopeni."

إِذْ دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلٰمًا قَالَ إِنَّا مِنْكُمْ وَجِلُونَ ﴿٥٢﴾

53. Wakasema: "Usiogope. Sisi tunakupa khabari njema ya (kuwa utazaa) mtoto mwenye ilimu kubwa."

قَالُوا لَا تَوْجَلْ إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلٰمٍ عَلِيمٍ ﴿٥٣﴾

54. Akasema: "Oh! Mnanipa khabari hii, na hali yakuwa uzee umenishika! Basi kwa njia gani mnanipa khabari njema hiyo?"

قَالَ أَبَشَّرْتُمُونِي عَلٰٓى أَنْ مَسَّنِيَ الْكِبَرُ فَبِمَ تُبَشِّرُونَ ﴿٥٤﴾

55. Wakasema: "Tumekupa khabari njema iliyo haki; basi usiwe miongoni mwa wanaokata tamaa."

قَالُوا بَشَّرْنٰكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُنْ مِنَ الْقٰنِطِينَ ﴿٥٥﴾

56. Akasema: "Na nani anayekata tamaa ya rehema ya Mola wake isipokuwa wale waliopotea?"

قَالَ وَمَنْ يَقْنَطُ مِنْ رَحْمَةِ رَبِّهِٓ إِلَّا الضَّآلُّونَ ﴿٥٦﴾

57. Akasema: "(Tena) kusudi lenu (jengine) ni nini enyi mliotumwa?"

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٥٧﴾

58. Wakasema: "Hakika sisi tumetumwa kwa wale watu wakosa (tukawaangamize)." (Watu wa Nabii Luti.)

قَالُوٓا إِنَّآ أُرْسِلْنَآ إِلٰى قَوْمٍ مُجْرِمِينَ ﴿٥٨﴾

59. "Isipokuwa waliomfuata Luti. Bila shaka sisi tutawaokoa wote hao (waliomfuata Luti)"

إِلَّآ اٰلَ لُوطٍ إِنَّا لَمُنَجُّوهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٩﴾

60. "Isipokuwa mkewe. Tunapimia yakuwa atakuwa miongoni mwa watakaokaa nyuma (waangamizwe)."

إِلَّا امْرَأَتَهُ قَدَّرْنَآ إِنَّهَا لَمِنَ الْغٰبِرِينَ ﴿٦٠﴾

---

50. Mwenyezi Mungu ana yote mawili. Upole kwa wanaostahiki upole, na Ukali kwa wanaostahiki ukali. Lakini upole ndio mkubwa kabisa sana sana, kwa hivi anawasamehe wengi hapa duniani na atawasamehe wengi kabisa huko Akhera, ila waliopindukia mipaka.

59. Nabii Ibrahimu na Nabii Luti walikuwa Mitume wakati mmoja lakini nchi mbali mbali, bali na Nabii Ismaili pia mwisho wake, na Nabii Is-haqa.

Nabii Ibrahimu alikuwa Shamu (Syria) na Nabii Luti Falastini (Israili sasa) na Nabii Ismaili Hijazi, na Nabii Is-haqa Shamu kama baba yake.

60. Mkewe Nabii Luti—kama mke wa Nabii Nuhu—walikuwa ni makafiri, na waume zao ni Mitume, na hali ya kuwa waume zao hawana habari ya haya na hali ya kuwa wanalala nao na kuamka nao kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 10 ya *Suratut Tahrym.*

Na kuna watu huwadaia vipenzi vyao kuwa wanajua yaliyo ndani ya vifua vya watu wanaokutana nao na watu wanaokuja kuwatazama na watu wanaokaa nao!

Basi ni uwongo kabisa maneno hayo. Anayejua yaliyofichikana katika vifua vya viumbe ni Mwenyezi Mungu tu kama anavyosema Mwenyewe mara kwa mara haya katika Qurani kuwa "Yeye (tu) ndiye anayejua yaliyo vifuani (mwa viumbe)."

61. Basi wajumbe walipofika kwa watu wa Luti (kwa sura za Kibinadamu)

فَلَمَّا جَآءَ ءَالَ لُوطٍ ٱلْمُرْسَلُونَ ﴿٦١﴾

62. (Luti) alisema: "Hakika nyinyi ni watu msiojulikana (na mimi; sikujuini)."

قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٦٢﴾

63. Wakasema: "Basi sisi tumekuletea yale ambayo walikuwa wanayafanyia shaka, (nayo ni maangamizo yao)."

قَالُوا بَلْ جِئْنَٰكَ بِمَا كَانُوا فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٣﴾

64. "Na tumefika kwako kwa (hilo jambo la) haki (la kuangamizwa), na hakika sisi ni wenye kusema kweli.

وَأَتَيْنَٰكَ بِٱلْحَقِّ وَإِنَّا لَصَٰدِقُونَ ﴿٦٤﴾

65. "Basi ondoka na watu wako katika kipande cha usiku (pingapinga la usiku), na wewe ufuate nyuma yao; wala yoyote katika nyinyi asigeuke nyuma (atakaposika shindo hilo la adhabu itakayoteremka, asije akatoka roho kwa kuona adhabu hiyo); na mwende (upesi upesi) mnakoamrishwa."

فَأَسْرِ بِأَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ ٱلَّيْلِ وَٱتَّبِعْ أَدْبَٰرَهُمْ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنكُمْ أَحَدٌ وَٱمْضُوا حَيْثُ تُؤْمَرُونَ ﴿٦٥﴾

66. Na tukamkatia (Nabii Luti) jambo hili; la kwamba mizizi yao itakatwa asubuhi (yaani wataangamiziliwa mbali asubuhi).

وَقَضَيْنَآ إِلَيْهِ ذَٰلِكَ ٱلْأَمْرَ أَنَّ دَابِرَ هَٰٓؤُلَآءِ مَقْطُوعٌ مُّصْبِحِينَ ﴿٦٦﴾

67. Na wakaja (kwa Luti) watu wa mji, hali ya kuwa wamefurahi (kuona wamekuja wageni wanaopendeza ili wawafanye machafu).

وَجَآءَ أَهْلُ ٱلْمَدِينَةِ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٦٧﴾

68. Akasema Nabii Luti: "Hakika hawa ni wageni wangu, msinifedheheshe"

قَالَ إِنَّ هَٰٓؤُلَآءِ ضَيْفِى فَلَا تَفْضَحُونِ ﴿٦٨﴾

69. "Na muogopeni Mwenyezi Mungu, wala msinidhalilishe (mbele yao)."

وَٱتَّقُوا ٱللَّهَ وَلَا تُخْزُونِ ﴿٦٩﴾

70. Wakasema (kumwambia Nabii Luti): "Je! Sisi hatukukutaza (kukaribisha) watu (wa nje)?"

قَالُوٓا أَوَلَمْ نَنْهَكَ عَنِ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٧٠﴾

71. Akasema: "Hawa (wanawake wote ni kama) binti zangu; ikiwa nyinyi ni wafanyao (yaliyoamrishwa basi waoeni, Msiwatake wanaume wenzenu)."

قَالَ هَٰٓؤُلَآءِ بَنَاتِىٓ إِن كُنتُمْ فَٰعِلِينَ ﴿٧١﴾

72. Naapa kwa umri wako! Hakika wao walikuwa katika ulevi wao (wa maovu); wanahangaika ovyo.

لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِى سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٢﴾

---

Na alimwambia Mtume wake Nabii Muhammad kuwa hayajui yaliyo katika vifua vya Masahaba zake — kuna wengine wanafiki, na yeye hawatambui. Alimwambia haya katika Aya ya 101 ya *Surati Tawba* kwa maneno haya: "Na katika wenyeji wa Madina pia (kuna wengine wanafiki); wamebobea katika unafiki; wewe huwajui (kuwa wanafiki). Sisi tunawajua."

Basi hana ruhusa Mwislamu kumpa mtu mwengine sifa hiyo ya Mwenyezi Mungu, si Uislamu kufanya hivyo.

67. Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 68 wamegeuza, makusudi, muradi wao "Wakifurahi," kama walivyogeuza katika Aya waliyoifanya kuwa ni ya 80 ya *Surat Hud*, ili kuwapigania Qaumu, Luti.

73. Mara adhabu ikawakamata lilipotoka jua (tu)

فَأَخَذَتْهُمُ الصَّيْحَةُ مُشْرِقِينَ ٧٣

74. Basi tukaifanya (miji ile chini juu) juu yake kuwa chini yake: Na tukawamiminia mvua ya mawe ya udongo wa motoni.

فَجَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ ٧٤

75. Hakika katika (masimulizi) haya yamo mazingatio (makubwa) kwa watu wenye kupima mambo.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْمُتَوَسِّمِينَ ٧٥

76. Na (miji) hii (tuliyoiangamiza hivi) iko katika njia zipitwazo (nao kila wakati; wanaona alama hizo).

وَإِنَّهَا لَبِسَبِيلٍ مُّقِيمٍ ٧٦

77. Bila shaka katika haya yamo mazingatio (makubwa) kwa wanaoamini.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ٧٧

78. Na hakika watu wa Kichakani (pia) walikuwa madhalimu; (nao ni watu wa Nabii Shuebu)

وَإِن كَانَ أَصْحَابُ الْأَيْكَةِ لَظَالِمِينَ ٧٨

79. Kwa hivyo tukawaadhibu; na nchi mbili hizi ziko katika njia zilizo dhahiri (wanazipita hao Makureshi makafiri katika misafara yao).

فَانتَقَمْنَا مِنْهُمْ وَإِنَّهُمَا لَبِإِمَامٍ مُّبِينٍ ٧٩

80. Na bila shaka wakazi wa (nchi ya) Hijri (pia) waliwakadhibisha Mitume (Mtume wao ni Nabii Salehe).

وَلَقَدْ كَذَّبَ أَصْحَابُ الْحِجْرِ الْمُرْسَلِينَ ٨٠

81. Na tuliwapa maonyo yetu; lakini walikuwa wakiyapuza.

وَآتَيْنَاهُمْ آيَاتِنَا فَكَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ٨١

82. Nao walikuwa wakichonga majumba katika majabali kwa amani. (Walikuwa wakichonga majabali kufanya majumba humo).

وَكَانُوا يَنْحِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا آمِنِينَ ٨٢

83. Basi ukelele wa adhabu ukawafikia asubuhi

فَأَخَذَتْهُمُ الصَّيْحَةُ مُصْبِحِينَ ٨٣

84. Hayakuwafaa (mali) waliyokuwa wakiyachuma (wala mambo waliyokuwa wakiyafanya).

فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ ٨٤

85. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake (vyote hivi) ila kwa ajili ya (kudhihirisha) haki. Na bila shaka Kiama kitafika. Basi msamehe msamaha mzuri (kila anayekufanyia ubaya; malipo yenu mtayakuta huko Kiama).

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ وَإِنَّ السَّاعَةَ لَآتِيَةٌ ۖ فَاصْفَحِ الصَّفْحَ الْجَمِيلَ ٨٥

86. Hakika Mola wako ndiye Muumbaji (na ndiye) Mjuzi.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ٨٦

87. Na tumekupa (hizi Aya) saba (tukufu za Alfatiiha—za Alhamdu) zisomwazo mara kwa mara, na (tumekupa) Qurani (yote nzima hii) tukufu.

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنَ الْعَظِيمَ ٨٧

---

78. Nabii Shuebu alipelekwa kwa watu wa Lubnani (Lebanon) hao Maphonecians tunaowasikia. Na nchi hii ni nchi ya miti mingi mpaka leo na nchi ya watu waliokuwa mahodari wa biashara na kwenda nchi za mbali mbali. Na mpaka leo sifa hii wanayo.

88. Usinyoshe (usikodowe) macho yako (kutazama) yale tuliyowastareheshea makundi mbali mbali ya hao (wabaya); wala usiwahuzunikie (huzuni kubwa ya kujiumiza nafsi yako); na inamisha bawa lako kwa wanaoamini (uwafunike kama kuku na ndege wengine wanavyofunika watoto wao. Yaani kuwa na huruma na hawa).

لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِۦٓ أَزْوَٰجًا مِّنْهُمْ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَٱخْفِضْ جَنَاحَكَ لِلْمُؤْمِنِينَ ٨٨

89. Na sema: "Hakika mimi ni Muonyaji niliye dhahiri (sifichi lolote).

وَقُلْ إِنِّىٓ أَنَا ٱلنَّذِيرُ ٱلْمُبِينُ ٨٩

90. Kama tulivyowateremshia (adhabu wote) waliojigawanya makundi (yakashindana katika kuupinga Uislamu)

كَمَآ أَنزَلْنَا عَلَى ٱلْمُقْتَسِمِينَ ٩٠

91. Ambao wameifanya Qurani kuwa ni mkusanyiko wa uwongo (aliokusanya Nabii Muhammad akadai kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu).

ٱلَّذِينَ جَعَلُوا۟ ٱلْقُرْءَانَ عِضِينَ ٩١

92. Basi ndivyo Wallahi tutakavyowauliza wote (hao siku ya Kiama).

فَوَرَبِّكَ لَنَسْـَٔلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ٩٢

93. Juu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

عَمَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ٩٣

94. Basi (wewe) yatangaze uliyoamrishwa (wala usijali upinzani wao) na ujitenge mbali na (vitendo vya) hao washirikina.

فَٱصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ ٱلْمُشْرِكِينَ ٩٤

95. Hakika sisi tunakutosha kukukingia (shari ya) wanaofanya dhihaka

إِنَّا كَفَيْنَٰكَ ٱلْمُسْتَهْزِءِينَ ٩٥

96. Wanaojaalia pamoja na Mwenyezi Mungu, waungu wengine. Basi karibuni hivi watajua.

ٱلَّذِينَ يَجْعَلُونَ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ٩٦

97. Na kwa yakini Sisi tunajua ya kwamba kifua chako kinadhikika kwa yale wasemayo (na wafanyayo katika kuipinga dini ya Uislamu).

وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّكَ يَضِيقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ ٩٧

98. (Lakini stahmili) umtukuze Mola wako pamoja na kumsifu (kwa sifa zake njema), na uwe miongoni mwa (hao wanaosifiwa kuwa) wanamsujudia (Mwenyezi Mungu).

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُن مِّنَ ٱلسَّٰجِدِينَ ٩٨

---

88. Mwenyezi Mungu amemsifu Mtume Muhammad katika mwisho wa *Suratit Tawba* kwa kuwa Yeye kwa uma wake ni kama mzazi rahimu kwa wanawe, anakatika maini akiona wanawe anaowapenda wanaingia mashakani au wanajitia mashakani. Kwa hivyo akihuzunika kweli kweli na akiungulika kweli kweli kuona watu hawataki kufuata uwongofu, wanapapia upotofu. Huzuni hiyo ilikuwa ikimuumiza moyo wake kweli kweli na ikiathiri siha yake hata akikaribia kuatilika. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu alimkariria mara kwa mara kuwa asifanye huzuni hizo, kama vile kumwambia *Falaallaka Bakhiun* au *Falaa Tahzan Alayhim* au *Falaa Tadhhab nafsuka Alayhim Hasaratin.*

97. Hakuna anayetukanwa asione taabu. Lakini aliambiwa astahamili. Na yeye akistahamili Hajibizani nao. Basi nasi tuwe vivi hivi. Tustahamili hata tukiona taabu vipi. Mstahamilivu hula mbivu kama alivyokula Mtume Muhammad na wenziwe wenginewe.

99. Na umuabudu Mola wako mpaka ikufikie hiyo yakini. (Nayo ni Mauti).

وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتّٰى يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿٩٩﴾

---

99. Waongo kabisa hao wanaojita mawalii na wakasema wamefikilia daraja kubwa ya kutopasiwa kufanya ibada. Mtume mwenyewe hakupewa jambo hilo — lisilokuwa na maana — watapewa wao. Hao maasi waliobobea katika uasi.

Na kuna wengineo wanaoasi dhahiri shahiri, na watu wao wakasema "Machoni mwetu tu ndio tunaona maasi haya, lakini katika hakika yake si maasi hayo!" Wanafiki wakubwa hao na wazandiki — wao na hao wanaowapigania.

ایاتها ۱۲۸ (۱۶) سُورَةُ النَّحْلِ مَكِّيَّةٌ (۷۰) رکوعاتها ۱۶

*Ina Aya 128* **SURATUN ' NAHL** *Ina Makara 16*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Amri ya Mwenyezi Mungu itafika (tu); basi msiihimize; (Muitakidi kuwa) Yeye (Mwenyezi Mungu) katakasika na kila mapungufu na Katukuka na ushirikina wa (hao makafiri).

2. Huwateremsha Malaika na Wahyi (kuihuisha Sharia) kwa amri yake (Mwenyezi Mungu) juu ya anaowataka katika waja wake kwamba "Waonyeni (viumbe) kuwa hakuna wa kuabudiwa isipokuwa Mimi, basi Niogopeni."

3. Ameziumba mbingu na ardhi kwa (ajili ya kudhihirisha) haki; ametukuka na ushirikina wao (hao makafiri).

4. Amemuumba mwanaadamu kwa tone la manii. Tahamaki amekuwa mshindani dhahiri (wa kumkataa Mwenyezi Mungu).

5. Na (pia) amewaumba wanyama. Katika hao mnapata (vifaa vitiavyo) joto na manufaa (mengine); na wengine mnawala.

6. Na mnaona raha mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni asubuhi.

7. Na (wanyama hao pia) hubeba mizigo yenu kupeleka katika miji msiyoweza kuifika isipokuwa kwa mashaka na taabu. Hakika Mola wenu ni Mpole sana (na) Mwenye rehema nyingi.

8. Na (amewaumba) farasi na nyumbu na punda ili muwapande na (wawe) mapambo. Na ataumba (vipando vyengine) msivyovijua. (Nayo ndio haya mamotokari, meli, ma. . . . .)

9. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu (kuonyesha) njia (iliyo sawa). Na ziko (nyingine zisizo sawa. (Basi

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

أَتَىٰ أَمْرُ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ ۚ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ
عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١﴾
يُنَزِّلُ الْمَلَائِكَةَ بِالرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ
مِنْ عِبَادِهِ أَنْ أَنْذِرُوا أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا
فَاتَّقُونِ ﴿٢﴾
خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ تَعَالَىٰ عَمَّا
يُشْرِكُونَ ﴿٣﴾
خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ
مُبِينٌ ﴿٤﴾
وَالْأَنْعَامَ خَلَقَهَا ۗ لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ وَمَنَافِعُ
وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٥﴾
وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ حِينَ تُرِيحُونَ وَحِينَ تَسْرَحُونَ ﴿٦﴾
وَتَحْمِلُ أَثْقَالَكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَمْ تَكُونُوا بَالِغِيهِ
إِلَّا بِشِقِّ الْأَنْفُسِ ۚ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٧﴾
وَالْخَيْلَ وَالْبِغَالَ وَالْحَمِيرَ لِتَرْكَبُوهَا وَزِينَةً ۚ
وَيَخْلُقُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨﴾
وَعَلَى اللَّهِ قَصْدُ السَّبِيلِ وَمِنْهَا جَائِرٌ ۚ

---

Mwanzo wa Sura hii wamepachikapachika hata wakasema mwisho wake:– "Ulimwengu wote unategemea Wahyi ili uendelee vizuri". Wamepachika haya ili kumdaia Wahyi Mkadiyani wao. Na ukafiri huu tumeurejeza katika marejezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na ya 4 ya *Suratul Baqarah* na mahala pengi penginepo. Wakatia ukafiri huu tena katika Aya yake ya kwanza waliyoifanya kuwa ni ya pili.

8. Qurani haikuacha kuashiria lolote lile japo kwa ufupi.

9. Tumekwisha kusema habari hii katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am.*

وَلَوْ شَاءَ لَهَدَاكُمْ أَجْمَعِينَ ⑨

nyinyi fuateni hiyo njia ya sawa anayokuonyesheni Mwenyezi Mungu). Na kama angalipenda bila shaka angalikuongozeni nyinyi nyote (mkitaka msitake. Lakini kakupeni huria ya kuchagua mtakalo).

هُوَ الَّذِيٓ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً لَّكُمْ مِّنْهُ شَرَابٌ
وَّمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ ⑩

10. Yeye ndiye anayekuteremshieni maji kutoka mawinguni; kwa hayo mnapata kinywaji, na kwa hayo (inaota) mimea ambayo humo mnalisha (wanyama).

يُنْۢبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ وَالنَّخِيلَ وَ
الْأَعْنَابَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ ۭ إِنَّ فِي ذٰلِكَ لَاٰيَةً
لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُونَ ⑪

11. (Na kwa hayo) hukuotesheeni mimea (ya kila namna) na mizeituni na mitende na mizabibu na kila matunda. Na bila shaka katika hayo imo ishara kwa watu wenye kufikiri (kuwa yuko Mwenyezi Mungu).

وَسَخَّرَ لَكُمُ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۭ
وَالنُّجُومُ مُسَخَّرٰتٌۢ بِأَمْرِهِ ۭ إِنَّ فِي ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ
لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُونَ ⑫

12. Na amekutiishieni usiku na mchana, na jua na mwezi. (Vyote vimeumbwa kwa ajili ya maslaha yenu). Na (pia) nyota zimetiishwa kwa amri yake. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wenye akili

وَمَا ذَرَاَ لَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ۭ
إِنَّ فِي ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّذَّكَّرُونَ ⑬

13. Na (akakuumbieni) hivi alivyovitawanya katika ardhi vya rangi mbali mbali. Hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wanaosikia mauidha.

وَهُوَ الَّذِي سَخَّرَ الْبَحْرَ لِتَأْكُلُوا مِنْهُ
لَحْمًا طَرِيًّا وَّتَسْتَخْرِجُوا مِنْهُ حِلْيَةً
تَلْبَسُونَهَا ۚ وَتَرَى الْفُلْكَ مَوَاخِرَ فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا
مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ⑭

14. Na Yeye ndiye aliyeitiisha bahari ili humo mule daima kitoweo kipya (samaki), na mtoe humo mapambo mnayoyavaa (ya lulu na marijani na yaliyo kama haya). Na utaona marikebu zikipasua humo, ili mtafute fadhila zake (kwa kufanya biashara) na ili mpate kushukuru.

وَأَلْقٰى فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ وَأَنْهٰرًا
وَّسُبُلًا لَّعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ⑮

15. Na akaweka katika ardhi milima ili (ardhi) isiyumbeyumbe nanyi. Na (akaweka) mito na mabarabara ili mpate kuongoza (njia mnazozitaka)

وَعَلٰمٰتٍ ۭ وَبِالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ ⑯

16. Na (ameziweka) alama nyingine. Na kwa nyota (pia) wao wanafuata njia.

أَفَمَنْ يَّخْلُقُ كَمَنْ لَّا يَخْلُقُ ۭ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ⑰

17. Ati, yule anayeumba (Naye ni Mwenyezi Mungu) atakuwa sawa na wale wasiyoumba? Je! Hamkumbuki?

وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللّٰهِ لَا تُحْصُوهَا ۭ إِنَّ اللّٰهَ
لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ⑱

18. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamtaweza kuzihisabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا تُسِرُّونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ⑲

19. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha.

وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللّٰهِ لَا يَخْلُقُونَ
شَيْئًا وَّهُمْ يُخْلَقُونَ ⑳

20. Na wale ambao wanawaabudu wasiokuwa Mungu hawaumbi chochote (hao wala hawakupata kuumba) bali wao wameumbwa.

21. Ni wafu, hawahai (si wazima), na hawajui watafufuliwa lini (Basi vipi wanaabudiwa).

أَمْوَاتٌ غَيْرُ أَحْيَاءٍ ۖ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٢١﴾

22. Mungu wenu ni Mungu mmoja. Lakini wale wasioiamini Akhera nyoyo zao zinakataa; nao wanatakabari.

إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۚ فَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ قُلُوبُهُم مُّنكِرَةٌ وَهُم مُّسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٢﴾

23. Bila shaka Mwenyezi Mungu anajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Kwa hakika Yeye hawapendi wanaotakabari.

لَا جَرَمَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْتَكْبِرِينَ ﴿٢٣﴾

24. Na wanapoambiwa (makafiri): "Mola wenu ameteremsha nini (kwa Nabii Muhammad)?" Wanasema: "(Hakuteremshiwa chochote. Ni) hadithi za uwongo tu za (watu) wa zamani (anazosimulia)"

وَإِذَا قِيلَ لَهُم مَّاذَا أَنزَلَ رَبُّكُمْ ۙ قَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٤﴾

25. (Wanapoteza watu hivi) ili wabebe mizigo (ya madhambi) yao kamili siku ya Kiama, na (pia) sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kuwa na ilimu (hao wanaowapoteza). Sikilizeni! Ni mibaya mno hiyo (mizigo) wanayoibeba.

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۙ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُم بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَزِرُونَ ﴿٢٥﴾

26. Walifanya hila wale waliokuwa kabla yao. Basi Mwenyezi Mungu akazisukua nyumba zao katika misingi, dari zikawaangukia juu yao; na ikawajia adhabu kutoka wasikokujua (yaani makafiri waliokuwa kabla yao, Mwenyezi Mungu alivibadilisha vitimbi vyao na akawaangamiza).

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَأَتَى اللَّهُ بُنْيَانَهُم مِّنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِن فَوْقِهِمْ وَأَتَاهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٦﴾

27. Kisha siku ya Kiama atawafedhehesha na atasema: "Wako wapi wale mliokuwa mkiwashirikisha na mimi ambao kwa ajili yao mlikuwa mkigombana (na Manabii)?" Watasema wale waliopewa ilimu: "Hakika fedheha na msiba leo utawafika makafiri"

ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يُخْزِيهِمْ وَيَقُولُ أَيْنَ شُرَكَائِيَ الَّذِينَ كُنتُمْ تُشَاقُّونَ فِيهِمْ ۚ قَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ إِنَّ الْخِزْيَ الْيَوْمَ وَالسُّوءَ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٢٧﴾

28. Ambao Malaika waliwafisha hali wamejidhulumu nafsi zao (kwa maasi yao). Basi watasalimu amri (kwa Mwenyezi Mungu waseme): "Hatukuwa tukifanya uovu wowote." (Ati wanamdanganya Mwenyezi Mungu. Malaika watawaambia):— "Ndiyo, hapana shaka Mwenyezi Mungu anajua sana mliyokuwa mkitenda."

الَّذِينَ تَتَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنفُسِهِمْ ۖ فَأَلْقَوُا السَّلَمَ مَا كُنَّا نَعْمَلُ مِن سُوءٍ ۚ بَلَىٰ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٨﴾

---

21. Katika hii Aya waliyoifanya kuwa ya 22 wametia upinzani wao wa kufa Nabii Isa. Na haya tumeyajibu katika majibisho ya Aya ya 55 ya *Surat Aali Imran* na Aya ya 159 ya *Suratun Nisaa* na mahala pengine.

24. Tazama wafujaji wanavyofuja, na hali ya kuwa wanajua kuwa ni maneno ya Mungu ya haki.

25. Wanaowapoteza watu wanachukua dhambi za maasi yao wanayoyafanya, na sehemu ya dhambi ya maasi yanayofanywa na wale waliowapoteza na waliowashajiisha katika mabaya. Katika kila maasi haya watapewa kiasi (per cent) chao makhsusi. Vikusanyike viparcent hivyo viwe zigo la kweli kweli liwaangamize. Haba na haba hujaza kibaba.

26-27. Si lazima vitimbi vya wenye kufanya vitimbi vifuzu. Mara nyingi haviwi au hugeuka vikawadhuru wenyewe; ikawa "Mchimba kisima huingia mwenyewe" na "Mla cha mwenziwe na chake huliwa." Na wakapata hizaya ya Akhera.

29. "Kwa hivyo ingieni milango ya Jahanamu kwa kukaa humo milele. Basi ni mabaya kabisa makazi ya wafanyao kiburi."

فَادْخُلُوٓا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خٰلِدِينَ فِيهَا ۖ فَلَبِئْسَ
مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٢٩﴾

30. Na wanapoambiwa wale wenye kumcha Mungu: "Ni nini aliyoteremsha Mola wenu?" Husema:- "(ametuteremshia) kheri (na kutwambia kuwa:- ) wale waliofanya wema katika dunia hii watapata wema, na hakika nyumba ya akhera ni nzuri kabisa; na ni bora kabisa nyumba (hiyo) ya wacha Mungu"

وَقِيلَ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا مَاذَآ أَنْزَلَ رَبُّكُمْ ۚ قَالُوا
خَيْرًا ۗ لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِى هٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ۚ
وَلَدَارُ الْاٰخِرَةِ خَيْرٌ ۚ وَلَنِعْمَ دَارُ الْمُتَّقِينَ ﴿٣٠﴾

31. Mabustani ya milele watayaingia; iwe inapita mbele yao mito; humo watapata watakacho. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu awalipavyo wenye kumcha

جَنّٰتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا تَجْرِى مِنْ تَحْتِهَا
الْأَنْهٰرُ لَهُمْ فِيهَا مَا يَشَآءُونَ ۚ كَذٰلِكَ
يَجْزِى اللَّهُ الْمُتَّقِينَ ﴿٣١﴾

32. Wale ambao Malaika huwafisha katika hali njema, wakasema: "Amani itakuwa juu yenu; ingieni Peponi kwa sababu ya yale (mema) mliyokuwa mkiyatenda."

الَّذِينَ تَتَوَفّٰىهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ طَيِّبِينَ ۙ يَقُولُونَ
سَلٰمٌ عَلَيْكُمُ ادْخُلُوا الْجَنَّةَ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٢﴾

33. Wanangoja jengine hawa (makafiri) ila Malaika wawafikie (kuwaangamiza) au iwafike amri ya Mola wako (ya kuwaadhibu)? Kama hivyo walifanya wale waliokuwa kabla yao. Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu; lakini walijidhulumu wenyewe.

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّآ أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ
أَوْ يَأْتِىَ أَمْرُ رَبِّكَ ۚ كَذٰلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ
قَبْلِهِمْ ۚ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلٰكِنْ كَانُوٓا
أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٣٣﴾

34. Basi ukawafikia uovu wa yale waliyoyafanya na ikawazunguka (adhabu) waliyokuwa wakiifanyia mzaha.

فَأَصَابَهُمْ سَيِّاٰتُ مَا عَمِلُوا وَحَاقَ بِهِمْ مَّا
ع كَانُوا بِهِۦ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٣٤﴾

35. Na wale washirikina wanasema: "Kama angalipenda Mwenyezi Mungu tusingaliabudu chochote badala yake, sisi (tusingefanya hivyo) wala baba zetu, wala tusingaliharimisha chochote bila Yeye (kututakia haya)." Basi kama hivi walifanya wale waliokuwa kabla yao. Basi kuna juu ya Mitume isipokuwa kufikisha (ujumbe) wazi wazi (tu basi)?

وَقَالَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَآءَ اللَّهُ مَا عَبَدْنَا مِنْ
دُونِهِۦ مِنْ شَىْءٍ نَّحْنُ وَلَآ اٰبَآؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِنْ
دُونِهِۦ مِنْ شَىْءٍ ۚ كَذٰلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ
فَهَلْ عَلَى الرُّسُلِ إِلَّا الْبَلٰغُ الْمُبِينُ ﴿٣٥﴾

---

35. Hivi ndivyo makafiri wanavyojitoa kimasomaso wanapofanya mabaya yao, hudai kuwa wameandikiwa, kwa hivyo hawana lawama. Na ndivyo baadhi ya Waislamu wengine wanavyojidai. Na hali ya kuwa sivyo hivyo. Mwenyezi Mungu amempa mtu akili ya kutambua jema na baya na kufanya alitakalo au kutolifanya. Qurani yote imejaa maneno namna haya:–

Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: Ya mwanamume na mwanamke, ili tufanyie mtihani (kwa amri zetu na makatazo yetu) kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona." Hakika sisi tumemuongoa, (tumembainishia) njia (zote mbili hizi; kuwa hii ndiyo ya kheri na hii ndiyo ya shari). Basi (mwenyewe tena) atakuwa mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru, (kukanusha); Kama ilivyo katika Aya ya pili na ya tatu za *Suratud Dahar;* "Na tukambainishia zote njia mbili — (iliyo njema na iliyo mbaya?"), kama ilivyo katika Aya ya kumi ya *Suratul Balad;* Na Thamudi tuliwaongoza lakini walipenda upofu kuliko kuongoka. Basi uliwatoa roho moto wa adhabu ifedheheshayo, kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma," kama ilivyo katika Aya ya 17 ya *Haa Mym Sajda;* Na "Ameifahamisha (Mwenyezi Mungu kila nafsi) uovu wake na kucha Mungu kwake. Basi Atafuzu kila mwenye kuitakasa nafsi yake hiyo; na ataharibikwa mwenye kuiviza" kama ilivyo katika Aya ya nane na tisa za *Surat Ash-shams.* Basi wasijidai watu kuwa 'Ah. Tumeandikiwa haya! Tufanyeje? Hatuna hila ila tufanye.' Basi ni kisingizio cha uwongo tu hicho.

36. Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila uma ya kwamba "Muabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni (Iblisi) muovu." Basi wako miongoni mwao ambao Mwenyezi Mungu amewaongoa, na wako miongoni mwao ambao upotofu (upotevu) umethubutu juu yao. Basi tembeeni katika ardhi na mwangalie ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ۖ فَمِنْهُم مَّنْ هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُم مَّنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ ۚ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿٣٦﴾

37. Ukiwa na hima kubwa ya kutaka kuwaongoza, lakini Mwenyezi Mungu hamuongozi yule anayepoteza (wengine). Wala hawatawapata wa kuwanusuru.

إِن تَحْرِصْ عَلَىٰ هُدَاهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَن يُضِلُّ ۖ وَمَا لَهُم مِّن نَّاصِرِينَ ﴿٣٧﴾

38. Nao (wakaapa) kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa kiapo chao cha nguvu (kwamba) Mwenyezi Mungu hatawafufua wafao. Kwa nini (asiwafufue)? Ni ahadi iliyolazimika kwake (kuwafufua na kuwalipa), lakini watu wengi hawajui.

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۙ لَا يَبْعَثُ اللَّهُ مَن يَمُوتُ ۚ بَلَىٰ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

39. (Atawafufua) ili kuwabainishia yale waliyokhitilafiana, na ili wajue waliokufuru ya kwamba wao walikuwa ni waongo.

لِيُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي يَخْتَلِفُونَ فِيهِ وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ كَانُوا كَاذِبِينَ ﴿٣٩﴾

40. Kauli yetu kwa kitu tunachokitaka (kiwe), ni kukiambia: "Kuwa;" basi kinakuwa tu.

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَن نَّقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٤٠﴾

41. Na wale waliohama (makwao) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baada ya kudhulumiwa huko, bila shaka tutawakalisha katika dunia kwa wema; na ujira wa akhera (unaowangojea) ni mkubwa zaidi; laiti kuwa (hawa wabaya) wanajua!

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي اللَّهِ مِن بَعْدِ مَا ظُلِمُوا لَنُبَوِّئَنَّهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَلَأَجْرُ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ ۚ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾

42. (Hao watakaopata hayo ni) wale wanaosubiri na wakamtegemea Mola wao.

الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٤٢﴾

43. Nasi hatukuwapeleka (kuwa Mitume) kabla yako isipokuwa wanaume ambao tuliwafunulia Wahyi. Basi waulizeni wenye kumbukumbu (za vitabu vya Mwenyezi Mungu vya kale) ikiwa nyinyi hamjui.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُّوحِي إِلَيْهِمْ ۚ فَاسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾

44. (Tuliwaleta) kwa ishara zilizo wazi na kwa vitabu. Na tumekuteremshia mauidha ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, na ili wapate kufikiri.

بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ ۗ وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٤﴾

45. Je! Wameaminisha wale wanaofanya hila mbaya kwamba Mwenyezi Mungu hatawadidimiza katika ardhi au haitawafika adhabu kutoka wasikokujua?

أَفَأَمِنَ الَّذِينَ مَكَرُوا السَّيِّئَاتِ أَن يَخْسِفَ اللَّهُ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٥﴾

---

37. Tumekwishabainisha katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am* na katika Aya ya 35 ya Sura hii.
45-57. Tumetaja katika Aya ya 26 ya Sura hii yanayowafika watu hawa.

46. Au hatawakamata (Mungu) katika kwenda kwao huko na huko, kisha hawataweza kuponyoka?

أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِي تَقَلُّبِهِمْ فَمَا هُم بِمُعْجِزِينَ ﴿٤٦﴾

47. Au hatawatesa kwa kuwapunguza kidogo kidogo? Hakika Mola wenu ni Mpole (na) Mwenye rehema.

أَوْ يَأْخُذَهُمْ عَلَىٰ تَخَوُّفٍ فَإِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٤٧﴾

48. Je! Hawavioni kila vitu alivyoumba Mwenyezi Mungu—ambavyo vivuli vyake vinazunguka kutoka kulia na kushoto—vinavyomsujudia Mwenyezi Mungu, hali ni vyenye kumnyenyekea?

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ يَتَفَيَّأُ ظِلَالُهُ
عَنِ الْيَمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِّلَّهِ وَهُمْ دَاخِرُونَ ﴿٤٨﴾

49. Na vinamsujudia Mwenyezi Mungu vyote vinavyokwenda mbinguni na katika ardhi; katika wanyama na Malaika pia, nao hawatakabari.

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مِن
دَابَّةٍ وَالْمَلَائِكَةُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٤٩﴾

50. Wanamuogopa Mola wao aliye juu yao, na wanatenda wanayoamrishwa.

يَخَافُونَ رَبَّهُم مِّن فَوْقِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٥٠﴾

51. Na Mwenyezi Mungu amesema: "Msifanye waungu wawili; hakika Yeye ni Mola Mmoja tu: basi Niogopeni Mimi tu."

وَقَالَ اللَّهُ لَا تَتَّخِذُوا إِلَٰهَيْنِ اثْنَيْنِ إِنَّمَا هُوَ إِلَٰهٌ
وَاحِدٌ فَإِيَّايَ فَارْهَبُونِ ﴿٥١﴾

52. Na ni vyake (peke yake vyote) vilivyomo katika mbingu na katika ardhi. Na ibada anastahiki yeye tu daima. Je! Mtamuogopa (mwingine) asiyekuwa Mwenyezi Mungu?

وَلَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَهُ الدِّينُ وَاصِبًا
أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَتَّقُونَ ﴿٥٢﴾

53. Na neema yoyote mliyonayo, basi imetoka kwa Mwenyezi Mungu. (Na nyinyi hamumshukuru). Kisha inapokuguseni dhara, mara yeye mnamlilia (mnamlalamikia).

وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمُ
الضُّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْأَرُونَ ﴿٥٣﴾

54. Kisha anapokuondoleeni hiyo dhara, mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha (tena) Mola wao.

ثُمَّ إِذَا كَشَفَ الضُّرَّ عَنكُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِّنكُم
بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾

55. Wanazikataa zile neema tulizowapa. Basi stareheni kidogo. Karibuni hivi mtajua (ubaya wenu).

لِيَكْفُرُوا بِمَا آتَيْنَاهُمْ فَتَمَتَّعُوا فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾

56. Na sehemu ya vile tulivyowaruzuku wanawawekea (waungu wao) wasiofahamu (wanayofanyiwa). Wallahi! (Kwa haki ya Mwenyezi Mungu) bila shaka nyinyi mtaulizwa juu ya yale mliyokuwa mkiyazua.

وَيَجْعَلُونَ لِمَا لَا يَعْلَمُونَ نَصِيبًا مِّمَّا رَزَقْنَاهُمْ
تَاللَّهِ لَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنتُمْ تَفْتَرُونَ ﴿٥٦﴾

---

53. Kila neema inayomfika kila kiumbe kaiumba Mungu, ima Mwenyewe au kwa wasita wa aliowaumba

56. Makafiri wakiwa na konde zao au wanyama wao basi walikuwa wakikata sehemu makhsusi wakisema "Hii itakuwa sehemu ya Mungu" (yaani itumike kusaidiwa masikini); na Hii itakuwa sehemu ya Masanamu tunayoyaabudu" (yaani wapelekewe wale wakubwa wa kutazama hayo masanamu) Basi ikitokea kuharibika ile sehemu ya masanamu huchukua ile sehemu ya Mungu wakaifanya ndiyo sehemu ya masanamu, na ile ya Mwenyezi Mungu wakaipuzilia mbali. Na ikitokea kuharibika ile ya Mwenyezi Mungu pia huipuzilia mbali (wakaumia masikini), hawaibadilishi kwa ile sehemu ya masanamu. Wakifanya hivi kama alivyosema haya Mwenyezi Mungu katika Aya ya 136 ya *Suratil An-am.*

57. Na wanamuwekea Mwenyezi Mungu mabinti; (kuwa kazaa watoto wanawake). Subhana! (Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo); hali wao wanajitakia wanaowapenda. (Nao ni watoto wanaume).

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ الْبَنَاتِ سُبْحَانَهُ وَلَهُم مَّا يَشْتَهُونَ ٥٧

58. Na mmoja katika wao anapopewa khabari ya (kuzaliwa kwake) mtoto wa kike, husawijika (husawidika) uso wake (huwa mweusi) akajaa sikitiko.

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ٥٨

59. (Akawa) anajificha na watu kwa sababu ya khabari mbaya ile aliyoambiwa! (Anafanya shauri!) Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni (kaburini, na hali ya kuwa mzima ili afe)? Sikilizeni! Ni mbaya mno hukumu yao hiyo.

يَتَوَارَىٰ مِنَ الْقَوْمِ مِن سُوءِ مَا بُشِّرَ بِهِ ۚ أَيُمْسِكُهُ عَلَىٰ هُونٍ أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ٥٩

60. (Waungu) wa wale wasioamini Akhera wana mifano mibaya (ya kupigiwa). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye sifa tukufu; naye ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ مَثَلُ السَّوْءِ ۖ وَلِلَّهِ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ ۚ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ٦٠ ع ١٢

61. Na lau Mwenyezi Mungu anawatesa (upesi) watu kwa sababu ya maasi yao; asingalimwacha hata mnyama mmoja juu ya ardhi; lakini anawaakhirisha mpaka muda uliowekwa. Na unapofika muda wao hawawezi kukawilia saa moja wala hawawezi kuutangulia.

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِظُلْمِهِم مَّا تَرَكَ عَلَيْهَا مِن دَابَّةٍ وَلَٰكِن يُؤَخِّرُهُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ لَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ٦١

---

Bali hawa wa sasa nao wanaojiita Waislamu wanafanya kama haya. Watayashughulikia yasiyokuwa kitu—kama mambo ya matanga—wakaacha yaliyokuwa kitu; au watayafanya yasiyokuwa bora zaidi—kama gharama za mahafali ya Maulidi—kuliko yaliyo bora zaidi, kama misikiti na vyuo. Na hata wakiambiwaje hawasikii. Wanasikia hayo wanayodanganyiwa, wakaacha ya Mwenyezi Mungu na Mtume, wanayoambiwa.

59. Walikuwa Waarabu wengine kabla ya Uislamu, akizaa mkewe mtoto mwanamke humuulia mbali. Akishakushikwa na uchungu huyo mwanamke huchimbwa shimo tayari chini ya miguu ya kitanda cha kuzalia au godoro au mkeka au . . . Akizaa mtoto mwanamume hupokewa kwa kofi na hoe hoe; lakini akizaa mwanamke huambiwa, 'Mpige teke mwenyewe humo shimoni.' Basi huwa hana la kufanya ila kumpiga teke humo; na hapo hapo hufukiwa na udhia ukajishia.

Ndiyo Mwenyezi Mungu anaitukana hukumu yao mbovu kabisa hii. Mtoto ni mtoto tu.

| | |
|---|---|
| Ukilea mwana mwema | Na mwana mui mlele |
| Mwema ukimpa chenga | Namui mpe chelele |
| Hujui mja kufaa | Mja kupa maji mbele |

Mui — Mbaya (kwa lugha ya watu wa zamani)
Mlele -- Mlee (Kwa lugha ya watu wa zamani)
Chelele — Chenga ndogo ndogo.

Na mpaka leo hii kuna watu wanaojiita Waislamu, na juu ya hivi wakizaa wake zao watoto wanawake, basi si kivumbi na kishindo na ugomvi na miachano inayotokea katika nyumba hizo! Uislamu gani huo! Wana makosa gani hao wanawake? Wao na hao waume zao sawa sawa.–

| | |
|---|---|
| Mambo yote ni ya Mungu | Atakalo ndilo huwa |
| Ndiye Pweke Mwenye Quwa | Mwenye amri amri na Shani |

Quwa — Nguvu

60. Kama vile kusema. "Wao ni madude tu hayaoni, hayasikii, hayasemi, hayatambui, hawana hata uhai."

61. Kuonyesha rehema ya Mwenyezi Mungu; hatesi upesi. Anawapa maasi muda mkubwa wa kuweza kurejea; yakiwafika baada ya hapo hawaambiwi pole.

62. Na wanampa Mwenyezi Mungu wanavyovichukia. (Nao ni watoto wanawake. Kumnasibishia kuwa amezaa watoto wanawake). Na ndimi zao zinasema uwongo kwamba wao (hao washirikina) watapata mema, (kwa Mwenyezi Mungu juu ya maneno yao hayo). Bila shaka wamewekewa Moto, nao wataachwa (humo).

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ وَتَصِفُ أَلْسِنَتُهُمُ
الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ الْحُسْنَىٰ ۖ لَا جَرَمَ أَنَّ لَهُمُ
النَّارَ وَأَنَّهُم مُّفْرَطُونَ ﴿٦٢﴾

63. Wallahi! Sisi tulituma (Mitume) kwa uma zilizokuwa kabla yako; lakini shetani aliwapambia vitendo vyao (vile vibaya wakaviona vizuri wakaendelea navyo). Kwa hivyo leo yeye (shetani) ni rafiki yao: (Lakini watachukiana naye kweli kweli Akhera), nao watapata adhabu iumizayo.

تَاللَّهِ لَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ
فَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَالَهُمْ فَهُوَ وَلِيُّهُمُ
الْيَوْمَ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾

64. Na hatukukuteremshia Kitabu (hiki) isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na (pia kiwe) uwongozi na rehema kwa watu wanaoamini.

وَمَا أَنزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ إِلَّا لِتُبَيِّنَ لَهُمُ
الَّذِي اخْتَلَفُوا فِيهِ ۙ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ
يُؤْمِنُونَ ﴿٦٤﴾

65. Na Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwa hayo akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika katika hayo imo ishara (ya kuonyesha kuweza kufufuliwa waliokufa. Ni ishara) kwa watu wasikiao.

وَاللَّهُ أَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ
بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ
يَسْمَعُونَ ﴿٦٥﴾

66. Na bila shaka katika wanyama muna mazingatio makubwa kwa ajili yenu. Tunakunywisheni katika vile vilivyomo matumboni mwao (vikitoka) baina ya choo na damu, (nayo ni maziwa; tukakunywisheni) maziwa safi mazuri kwa wanywao.

وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۖ نُّسْقِيكُم مِّمَّا
فِي بُطُونِهِ مِن بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَّبَنًا خَالِصًا
سَائِغًا لِّلشَّارِبِينَ ﴿٦٦﴾

67. Na katika matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza vinywewe vya ulevi (vinavyokatazwa) na mnapata riziki nzuri. Hakika katika hayo muna mazingatio kwa watu watumiao akili zao.

وَمِن ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالْأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ
سَكَرًا وَرِزْقًا حَسَنًا ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً
لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾

68. Na Mola wako akamfahamisha nyuki ya kwamba "Jitengenezee majumba (yako) katika milima na katika miti na katika yale (majumba) wanayojenga (watu)."

وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى النَّحْلِ أَنِ اتَّخِذِي مِنَ
الْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُونَ ﴿٦٨﴾

69. Kisha "Kula katika kila matunda, na upite katika njia za Mola wako zilizofanywa nyepesi

ثُمَّ كُلِي مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ فَاسْلُكِي سُبُلَ

64. Tazama baadhi ya faida za kuteremshwa Qurani.

67. Sakarah hapa ni vinywewe vizuri kabla ya kufanyika ulevi au ulevi khasa. Na tamko hili halitokani na sukkar (sukari).

Katika mwaka 300 B.C. (kabla ya kuzaliwa Nabii Isa) ndipo kulipovumbuliwa Bara Hindi kufanya sukari katika miwa wakaita SAKKAR.

Kisha ujuzi wake ukatwawa na Maajami (Persians), tena Waarabu na wakaiita Sukkar. Mwisho ukenda kwa Wazungu, wakaiita Sugar.

Ama hii sukari miwa ya sasa imevumbuliwa mwaka 1811 (Beset-root Sugar).

68. Tunatajiwa neema ya kuumbiwa nyuki.

Wamepinduapindua katika aya hii waliyoifanya ya 69 ili wamdaie Utume mtu wao, na hali ya kuwa wanajua

رَبِّكِ ذُلُلًا ۚ يَخْرُجُ مِنْ بُطُوْنِهَا شَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ
أَلْوَانُهُ فِيْهِ شِفَآءٌ لِّلنَّاسِ ۗ إِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً
لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿٦٩﴾

(kuzipita)." Kinatoka katika matumbo yao kinywaji (asali) chenye rangi mbali mbali; ndani yake kina ponyo (poza) kwa wanaadamu. Hakika katika hayo muna mazingatio kwa watu wenye fikra.

وَاللّٰهُ خَلَقَكُمْ ثُمَّ يَتَوَفّٰىكُمْ ۙ وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّرَدُّ إِلٰٓى
أَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْ لَا يَعْلَمَ بَعْدَ عِلْمٍ شَيْئًا ۚ
إِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ قَدِيْرٌ ﴿٧٠﴾ ع ١٥

70. Na Mwenyezi Mungu amekuumbeni kisha anakufisheni; na miongoni mwenu wako wanaorudishwa katika umri mbaya (wa uzee kabisa). Akawa hajui chochote (tena) baada ya (ule) ujuzi (aliokuwa nao). Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Muweza.

وَاللّٰهُ فَضَّلَ بَعْضَكُمْ عَلٰى بَعْضٍ فِي الرِّزْقِ ۚ
فَمَا الَّذِيْنَ فُضِّلُوْا بِرَآدِّيْ رِزْقِهِمْ عَلٰى مَا مَلَكَتْ
أَيْمَانُهُمْ فَهُمْ فِيْهِ سَوَآءٌ ۚ أَفَبِنِعْمَةِ اللّٰهِ
يَجْحَدُوْنَ ﴿٧١﴾

71. Na Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine katika riziki. Na wale waliofadhilishwa hawarudishi (hawawagawii) riziki zao kwa wale iliowatamalaki mikono yao ya kulia (watumwa wao); ili wawe sawa katika riziki hii. (Basi vipi nyinyi mnamfanya Mwenyezi Mungu sawa na waja wake, na nyinyi hamkubali kuwa sawa na watumwa wenu)? Basi je, wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمْ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَّجَعَلَ
لَكُمْ مِّنْ أَزْوَاجِكُمْ بَنِيْنَ وَ حَفَدَةً
وَّرَزَقَكُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ ۚ أَفَبِالْبَاطِلِ
يُؤْمِنُوْنَ وَبِنِعْمَتِ اللّٰهِ هُمْ يَكْفُرُوْنَ ﴿٧٢﴾

72. Na Mwenyezi Mungu amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na akakujaalieni kutoka kwa wake zenu watoto na wajukuu, na akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini yasiyokuwa ya haki na kuzikataa neema za Mwenyezi Mungu?

وَ يَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَهُمْ
رِزْقًا مِّنَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ شَيْئًا وَّلَا
يَسْتَطِيْعُوْنَ ﴿٧٣﴾

73. Na wanamwacha Mwenyezi Mungu wakawaabudu wasiowamilikia riziki hata kidogo si kutoka mbinguni wala katika ardhi, wala hawana uweza wa lolote.

فَلَا تَضْرِبُوْا لِلّٰهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ وَ
أَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٧٤﴾

74. Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu anajua, na nyinyi hamjui (lolote).

ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا عَبْدًا مَّمْلُوْكًا لَّا يَقْدِرُ عَلٰى
شَيْءٍ وَّمَنْ رَّزَقْنٰهُ مِنَّا رِزْقًا حَسَنًا فَهُوَ
يُنْفِقُ مِنْهُ سِرًّا وَّجَهْرًا ۖ هَلْ يَسْتَوٗنَ ۚ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ ۚ
بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٧٥﴾

75. Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa mtumwa anayemilikiwa, asieweza chochote, na (mwingine) tuliyemruzuku riziki njema inayotoka kwetu, naye akawa anatoa katika riziki hiyo kwa siri na dhahiri. Je, watakuwa sawa? (Basi vipi mnamfanya Mwenyezi Mungu sawa na masanamu?) Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu. Lakini wengi katika wao hawajui.

وَضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا رَّجُلَيْنِ أَحَدُهُمَا أَبْكَمُ لَا

76. Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa

---

kuwa Wahyi huu uliotajiwa nyuki ni Ilhamu tu, sio Wahyi wa kujiwa na Malaika wala kusemezwa na Mwenyezi Mungu.

71. Wao hawawakubali watumwa wao kuwa washirika wao, na wao wanamthubutishia Mwenyezi Mungu washirika katika waja wake.

72. Katika neema kubwa kabisa ni kuzaa ukabarikiwa. Basi shukuru sana sana.

73. Wazimu wao wa kuwaomba wasiokuwa Mwenyezi Mungu.

يَقْدِرُ عَلَىٰ شَيْءٍ وَهُوَ كَلٌّ عَلَىٰ مَوْلَاهُ أَيْنَمَا
يُوَجِّههُّ لَا يَأْتِ بِخَيْرٍ هَلْ يَسْتَوِي هُوَ وَمَن
ع يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَهُوَ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٧٦﴾
١٦

watu wawili (wengine). Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo juu ya bwana wake, popote amwelekezapo haleti kheri. Je! Huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu, naye yuko juu ya njia iliyonyoka?

وَلِلَّهِ غَيْبُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ
إِلَّا كَلَمْحِ الْبَصَرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٧٧﴾

77. Na iko kwa Mwenyezi Mungu tu siri ya mbinguni na vilivyo katika ardhi; wala halikuwa hilo jambo la (kufika) saa (ile ya Kiyama) ila ni kama kupepesa jicho au ni karibu zaidi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

وَاللَّهُ أَخْرَجَكُم مِّن بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ لَا تَعْلَمُونَ
شَيْئًا وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ
وَالْأَفْئِدَةَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٨﴾

78. Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui chochote, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mupate kushukuru.

أَلَمْ يَرَوْا إِلَى الطَّيْرِ مُسَخَّرَاتٍ فِي جَوِّ السَّمَاءِ
مَا يُمْسِكُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ
يُؤْمِنُونَ ﴿٧٩﴾

79. Je! Hawawaoni ndege wanavyotumishwa (utumwa wa Mwenyezi Mungu) katika anga la mbingu? Hakuna awazuiaye (angani wasianguke) isipokuwa (Mwenyewe) Mwenyezi Mungu. Bila shaka katika hayo yamo mazingatio kwa watu wanaoamini.

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِّن بُيُوتِكُمْ سَكَنًا وَجَعَلَ
لَكُم مِّن جُلُودِ الْأَنْعَامِ بُيُوتًا تَسْتَخِفُّونَهَا
يَوْمَ ظَعْنِكُمْ وَيَوْمَ إِقَامَتِكُمْ وَمِنْ أَصْوَافِهَا
وَأَوْبَارِهَا وَأَشْعَارِهَا أَثَاثًا وَمَتَاعًا إِلَىٰ
حِينٍ ﴿٨٠﴾

80. Na Mwenyezi Mungu amekujaalieni majumba yenu yawe makazi (yenu). Na (pia) amekujaalieni (kuweza kufanya) nyumba kwa ngozi za wanyama (Nazo ni mahema) mnayoyaona mepesi (kuyachukua) wakati wa safari zenu na wakati wa kutua kwenu. Na kwa sufu zao (wanyama), na manyoya yao, na nywele zao, (mnatengeneza) vyombo na vifaa vya kutumia kwa muda mrefu.

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِّمَّا خَلَقَ ظِلَالًا وَجَعَلَ لَكُم
مِّنَ الْجِبَالِ أَكْنَانًا وَجَعَلَ لَكُمْ سَرَابِيلَ تَقِيكُمُ
الْحَرَّ وَسَرَابِيلَ تَقِيكُم بَأْسَكُمْ كَذَٰلِكَ يُتِمُّ
نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تُسْلِمُونَ ﴿٨١﴾

81. Na Mwenyezi Mungu katika vitu alivyoviumba amekufanyieni vitu viletavyo kivuli; na amekufanyieni maskani katika milima, na amekufanyieni kanzu zinazokukingeni na joto (na baridi, na amekufanyieni) nguo za chuma zinazokukingeni katika vita vyenu. Namna hivi anakutimizieni neema zake ili mupate kutii.

فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿٨٢﴾

82. Wakikengeuka, basi; si juu yako wewe ila kufikisha (ujumbe) wazi wazi (bila ya kuficha. Nawe umefikisha; basi hapana lawama juu yako).

يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ يُنكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ
ع الْكَافِرُونَ ﴿٨٣﴾
١٤

83. Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu, kisha wanazikanusha; na wengi katika wao ni makafiri.

وَيَوْمَ نَبْعَثُ مِن كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا ثُمَّ لَا يُؤْذَنُ

84. Na (wakumbushe) siku tutakapowainua mashahidi (wa kushuhudia) katika kila uma; kisha haitaruhusiwa kwa waliokufuru (kutoa udhuru) wala

78-81. Inatajwa Qudra ya Mwenyezi Mungu na uweza wake na neema zake, zizingatiwe zishukuriwe.

82. Imebainishwa mara nyingi kuwa kazi za Mitume na Waongozi ni kufikisha kuliko dhahiri, wakifuatwa, wasifuatwe.

hawataambiwa watake radhi (bali wataadhibiwa tu).

لِلَّذِينَ كَفَرُوا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٨٤﴾

85. Na wale waliodhulumu watakapoiona adhabu, (wakalia wakisikitika) hawatapunguziwa hiyo adhabu wala hawatapewa muda mwengine (wa kuja ulimwenguni kufanya mema badala ya yale mabaya).

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ ظَلَمُوا الْعَذَابَ فَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ
وَلَا هُمْ يُنْظَرُونَ ﴿٨٥﴾

86. Na waliomshirikisha Mungu watakapowaona hao waliowashirikisha na Mungu, watasema: "Mola wetu! Hawa ndio washirikishwa wetu ambao tulikuwa tukiwaabudu badala yako." Ndipo (wale walioshirikishwa) watakapowatupia neno hili hao (washirikina) kuwa: "Hakika nyinyi ni waongo!"

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ أَشْرَكُوا شُرَكَاءَهُمْ قَالُوا رَبَّنَا
هَٰؤُلَاءِ شُرَكَاؤُنَا الَّذِينَ كُنَّا نَدْعُو مِنْ دُونِكَ ۖ
فَأَلْقَوْا إِلَيْهِمُ الْقَوْلَ إِنَّكُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٨٦﴾

87. Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu, na yatawapotea waliyokuwa wakiyazua.

وَأَلْقَوْا إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ السَّلَمَ ۖ وَضَلَّ عَنْهُمْ
مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٨٧﴾

88. (Ama wale waliokufuru na kuwazuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu tutawazidishia adhabu juu ya adhabu, kwa kufisidi kwao.

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ
زِدْنَاهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا
يُفْسِدُونَ ﴿٨٨﴾

89. Na (wakumbushe) siku tutakapowainua mashahidi katika kila uma wanaowashuhudia kwa yanayotokana na wao (wawashuhudilie amali zao); na tukulete na wewe uwe shahidi juu ya hawa (uma wako). Na tumekuteremshia Kitabu hiki kielezacho kila kitu, na ambacho ni uwongofu na rehema, na khabari za furaha kwa wanaojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) Waislamu.

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِنْ
أَنْفُسِهِمْ ۖ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيدًا عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ ۚ
وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِكُلِّ شَيْءٍ
وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ ﴿٨٩﴾

90. Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu, na kufanya hisani, na kuwapa jamaa (na wengineo); na anakataza uchafu na uovu, na dhulma. Anakunasihini ili mupate kufahamu (mfuate).

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَاءِ ذِي
الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ
يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

91. Na timizeni ahadi mnazozitoa kwa jina la Mwenyezi Mungu mnapoahidi; wala msivunje hizo ahadi baada ya kuzithubutisha, hali mumekwisha mfanya Mwenyezi Mungu kuwa shahidi wenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua (yote) mnayoyafanya.

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْقُضُوا
الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ
كَفِيلًا ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٩١﴾

92. Wala msiwe kama yule mwanamke

وَلَا تَكُونُوا كَالَّتِي نَقَضَتْ غَزْلَهَا مِنْ بَعْدِ

86. Watakavyobamandukana, wafuatwa na wafuasi; kila mmoja anajipigania mwenyewe na kumdidimiza mwenziwe.

89. Zinabainishwa tena baadhi ya nafuu zilizopatikana kwa kuteremshwa Qurani.

90. Hii aya waliyoifanya ya 91, maelezo yake ya matamko matatu ya mema, mazuri. Ama katika kufasiri mabaya hawakusibu.

90-91. Baadhi ya maamrisho mazuri sana ya Qurani.

92. Huu ni mfano tu anaopigiwa anayevunja ahadi yake. Mfano wake kama mtu aliyepoteza nguvu zake barabara katika kusokota uzi au kamba; kisha akainyambulia mbali!

قُوَّةٍ أَنكَاثًا ۚ تَتَّخِذُونَ أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ
أَن تَكُونَ أُمَّةٌ هِيَ أَرْبَىٰ مِنْ أُمَّةٍ ۚ
إِنَّمَا يَبْلُوكُمُ اللَّهُ بِهِ ۚ وَلَيُبَيِّنَنَّ لَكُمْ يَوْمَ
الْقِيَامَةِ مَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٩٢﴾

aliyeukata uzi wake vipande vipande baada ya (kuusokota) kuwa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu njia ya kudanganyana baina yenu. Kwa ajili kundi moja la watu kuwa na nguvu zaidi kuliko kundi la watu wengine (ndio mnawaachia hao wasio na nguvu mliopeana ahadi nao! Msifanye hivyo). Hakika Mwenyezi Mungu anakujaribuni kwa njia hiyo. Na bila shaka atakubainishieni siku ya Kiyama mliyokuwa mkihitalifiana.

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَٰكِن يُضِلُّ
مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ ۚ وَلَتُسْأَلُنَّ عَمَّا
كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

93. Na Mwenyezi Mungu angalitaka, kwa yakini angalikufanyeni kundi moja tu (mnamtii nyote kama alivyowafanya Malaika. Lakini kakuacheni mfanye mtakavyo). Lakini anamuachia kupotea anayemtaka. Na anamwongoa anayemtaka. Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya (kwani mumepewa ujuzi wa kujua jema na baya na mkapewa nguvu ya kuweza kufanya mema mkaacha mabaya).

وَلَا تَتَّخِذُوا أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ فَتَزِلَّ قَدَمٌ
بَعْدَ ثُبُوتِهَا وَتَذُوقُوا السُّوءَ بِمَا صَدَدتُّمْ عَن
سَبِيلِ اللَّهِ ۖ وَلَكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٩٤﴾

94. Wala msifanye viapo vyenu ni njia ya kudanganyana baina yenu. Usije mguu ukateleza (ukaingia Motoni) baada ya kuthubutu, na mkaonja (jaza ya) maovu yenu kwa sababu ya kule kuwazuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, na mkapata adhabu kubwa.

وَلَا تَشْتَرُوا بِعَهْدِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۚ إِنَّمَا عِندَ
اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩٥﴾

95. Wala msiuze ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa thamani chache (mnayopata hapa ulimwenguni). Kilicho kwa Mwenyezi Mungu ndicho bora kwenu, ikiwa mnajua (jambo basi jueni na hili).

مَا عِندَكُمْ يَنفَدُ ۖ وَمَا عِندَ اللَّهِ بَاقٍ ۗ وَلَنَجْزِيَنَّ
الَّذِينَ صَبَرُوا أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا
يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾

96. Mlivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu (vya jaza yenu) ndivyo vitakavyobakia. Na kwa yakini sisi tutawapa waliosubiri ujira wao (mkubwa kabisa) kwa yale mazuri waliyokuwa wakiyatenda.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ
فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ
أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

97. Wafanyaji mema, wanaume au wanawake, hali yakuwa ni Waislamu, tutawahuisha maisha mema, na tutawapa ujira wao (Akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda.

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ
الرَّجِيمِ ﴿٩٨﴾

98. Na ukitaka kusoma Qurani piga Audhu (kwanza, jikinge) kwa Mwenyezi Mungu (akulinde) na Shetani aliyefukuzwa (katika rehema yake Mwenyezi Mungu Anza kwa kusoma Audhu).

إِنَّهُ لَيْسَ لَهُ سُلْطَانٌ عَلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَعَلَىٰ
رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٩٩﴾

99. Hakika yeye (Shetani) hana nguvu juu ya wale walioamini na wanaomtegemea Mola wao.

---

93. Tumebainisha haya katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am* Juzuu ya nane na Aya ya 35 ya Sura hii hii.

100. Unaona hapa Mwenyezi Mungu anavyodhihirisha wazi kabisa kuwa Shetani hana uweza wa kumtia mtu katika ma-asiya akitaka asitake. Tukimtii Shetani tunamtii kwa kutaka kwetu sio ametuzidi nguvu, ametutia pingu.

100. Nguvu zake ni juu ya wale wanaomfanya rafiki (wakamfuata), na juu ya wale wanaomshirikisha (Mwenyezi Mungu) naye.

إِنَّمَا سُلْطَٰنُهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُۥ وَٱلَّذِينَ هُم
بِهِۦ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٠﴾

101. Na tunapoibadili Aya kwa Aya (nyingine), na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anajua anayoyateremsha, wanasema: "Wewe ni mzushi tu! Bali wengi katika wao hawajui (lolote; wanajisemea wanayoyasikia kwa wakubwa wao tu).

وَإِذَا بَدَّلْنَآ ءَايَةً مَّكَانَ ءَايَةٍ ۙ وَٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا
يُنَزِّلُ قَالُوٓا۟ إِنَّمَآ أَنتَ مُفْتَرٍۭ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ
لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾

102. Sema: "Roho takatifu (yaani Jibrili) ameiteremsha kutoka kwa Mola wako kwa haki, ili kuwathubutisha wale walioamini, na kuwa uwongofu na khabari njema kwa waliosilimu.

قُلْ نَزَّلَهُۥ رُوحُ ٱلْقُدُسِ مِن رَّبِّكَ بِٱلْحَقِّ
لِيُثَبِّتَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَهُدًى وَبُشْرَىٰ
لِلْمُسْلِمِينَ ﴿١٠٢﴾

103. Na bila shaka tunajua kwamba wanasema: "Yuko mtu anayemfundisha." (Lakini) lugha ya yule wanayemwelekezea (kuwa anamfundisha Mtume) ni ya kigeni, na hii (lugha inayotumika katika Qurani) ni lugha ya Kiarabu bulbul.

وَلَقَدْ نَعْلَمُ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُۥ بَشَرٌ ۗ
لِّسَانُ ٱلَّذِى يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِىٌّ وَهَٰذَا
لِسَانٌ عَرَبِىٌّ مُّبِينٌ ﴿١٠٣﴾

104. Hakika wale wasioziamini Aya za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri kwani wenyewe hawataki). Basi watapata adhabu iumizayo.

إِنَّ ٱلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ ۙ
لَا يَهْدِيهِمُ ٱللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٤﴾

---

101. Wameyabadilisha makusudi, makusudio ya hii Aya waliyoifanya ni 102 kama walivyobadili makusudio ya Aya 106 ya *Suratul Baqarah* ili wakanushe habari ya Naskh. Na sisi tumewajibu katika Aya hiyo. Tazama uwongo wao.

Kila jambo likitaka kuletwa huletwa kidogo kidogo. Ndivyo kiakili. Sivyo kulivurumiza mara moja; itakuwa taabu kutiika au itakuwa muhali khasa.

Kama ulevi ulivyoanza kukatazwa katika Uislamu: kwanza ilishuka aya ya 219 ya *Suratul Baqarah* iliyosema kuwa ulevi una madhara makubwa kwa hao walewao kuliko faida wanayoipata hao wauzao. Lakini haikuambiwa msilewe.

Kisha ikashuka Aya ya 43 ya *Suratin Nisaa* iliyokataza mtu kusali na hali ya kuwa ana taathira bado ya ulevi kichwani; Ikawa takriba mchana kutwa mtu hawezi kulewa. Kwani akilewa baada ya Sala ya Adhuhuri, wakati utakapofika wa Laasiri utakuwa ulevi bado haujamtoka na lazima asali Laasiri. Basi kwa hivyo hathubutu kulewa baada ya Sala ya Adhuhuri. Na vile vile hathubutu kulewa baada ya Sala ya Laasiri kwa kuchelea Sala ya Magharibi. Na vile vile hathubutu kulewa baada ya Sala ya Magharibi kwa kuchelea Sala ya Isha.

Nafasi anaweza kupata hapo baada ya Sala ya Isha kwani unaweza kumtoka ulevi kabla ya Sala ya Alfajiri. Na nafasi pia labda anaweza kupata baada ya Sala ya Alfajiri kwani inamkinika kumtoka huo ulevi kabla ya Sala ya Adhuhuri; basi ikawa sasa muda mwingi amezuilika na kulewa; hata wengine wakaanza kuacha na wengine wakaacha khasa.

Baada ya kupita kitambo kirefu hivi mara iliteremka aya ya 90 ya *Suratil Maida* ya kuzuilia ulevi kabisa kabisa pasina kutolewa ruhusa hata wakati wowote ule.

Basi wale makafiri kwa kuona mkatazo mdogo namna huu — au muamrisho mdogo mdogo — ndio wakastaajabu wakasema Mbona mara hivi na mara hivi. Wajinga; hawatambui hikima hii au wanajitia pambani kusudi.

103. Kiunguja husema 'Akutukanaye hakuchagulii tusi;' hukuvurumizia hata lisilolingia akilini Basi ndivo Makureshi katika kumsambikizia Mtume kila tusi walisema: 'Maneno yake haya anayoyaita Qurani anafundishwa na Jabr.' Na huyu Jabr alikuwa muhunzi wa Kirumi aliyekuwa mtumwa wa baadhi ya Makuresh. Basi mtumwa, mja-na-maji, tena si Mwarabu, atajua kusema ya ufasihi namna haya yaliyomo katika Qurani ambayo hakuna kiumbe chochote anayeweza kuyasogelea kwa ufasihi wake? Lakini ndiyo hivyo kama inavyosemwa kuwa 'Akutukanaye hakuchagulii tusi.'

104. Wenyewe hawataki, kwa nini atawaongoza kwa nguvu, naye amewapa uweza (power) wa kufanya mema na mabaya, kama ilivyobainishwa katika Aya ya 125 ya *Suratul An-am* na Aya ya 35 ya Sura hii hii.

105. Wanaozua uwongo (wakipita wakitangaza kama hivyo kusema Mtume anafundishwa Qurani na huyo Mrumi) ni wale wasioziamini Aya za Mwenyezi Mungu; na hao ndio waongo.

106. Anayemkufuru Mwenyezi Mũngu baada ya Uislamu wake (inamngojea adhabu kubwa) isipokuwa yule aliyeshurutishwa, hali ya kuwa moyo wake umetuwa juu ya Uislamu (wake); lakini anayekifungulia ukafiri kifua chake, hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iko juu yao; na (watu namna hiyo) watapata adhabu kubwa.

107. Hayo (ya kuadhibiwa walioitakidi ukafiri) ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya dunia kuliko akhera, na kwa sababu Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

108. Hao ndio ambao (kama kwamba) amezifumba Mwenyezi Mungu nyoyo zao na masikio yao na macho yao. Na hao ndio walioghafilika kweli kweli.

109. Hakuna shaka ya kwamba hao ndio wenye khasara katika akhera.

110. Kisha hakika Mola wako, kwa wale waliohama (makwao) baada ya kuteswa, (hata wakasema yasiyofaa), kisha wakapigania dini na wakasubiri, bila shaka Mola wako baada ya hayo ni Mwingi wa msamaha na Mwingi wa rehema (juu yao).

111. (Wakumbushe) siku ambayo kila nafsi itakuja kujitetea; na kila nafsi italipwa (sawasawa na) amali ilizofanya; nao hawatadhulumiwa.

112. Na Mwenyezi Mungu anakupigieni mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiujia kwa wingi kutoka kila mahali. Lakini ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu, kwa hivyo Mwenyezi Mungu akauvika vazi la njaa na khofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

113. Na aliwajia Mtume miongoni mwao (wa jinsi moja na wao); lakini wakamkadhibisha; basi adhabu iliwafika, hali ya kuwa wenyewe wamejidhulumu.

114. Kuleni katika vile alivyokupeni Mwenyezi Mungu, vilivyo halali na vizuri. Na shukuruni

إِنَّمَا يَفْتَرِي الْكَذِبَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ
بِآيَاتِ اللَّهِ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿١٠٥﴾

مَنْ كَفَرَ بِاللَّهِ مِنْ بَعْدِ إِيمَانِهِ إِلَّا مَنْ أُكْرِهَ
وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ وَلَٰكِنْ مَنْ شَرَحَ
بِالْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِنَ اللَّهِ وَلَهُمْ
عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠٦﴾

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمُ اسْتَحَبُّوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ
وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿١٠٧﴾

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ طَبَعَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَسَمْعِهِمْ
وَأَبْصَارِهِمْ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٠٨﴾

لَا جَرَمَ أَنَّهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٠٩﴾

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ هَاجَرُوا مِنْ بَعْدِ مَا فُتِنُوا ثُمَّ
جَاهَدُوا وَصَبَرُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا
لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١١٠﴾

يَوْمَ تَأْتِي كُلُّ نَفْسٍ تُجَادِلُ عَنْ نَفْسِهَا
وَتُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَا عَمِلَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١١١﴾

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ آمِنَةً
مُطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا رِزْقُهَا رَغَدًا مِنْ كُلِّ
مَكَانٍ فَكَفَرَتْ بِأَنْعُمِ اللَّهِ فَأَذَاقَهَا اللَّهُ
لِبَاسَ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿١١٢﴾

وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِنْهُمْ فَكَذَّبُوهُ
فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١١٣﴾

فَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَالًا طَيِّبًا وَاشْكُرُوا

106. Tumeona namna gani Waislamu walivyokuwa wakiuawa kwa ajili ya dini yao, wakitambulikana na jamaa zao. Basi hapa wanapewa ruhusa waukatae Uislamu wao kwa ulimi wao tu hivi hapo wanapogunduliwa na jamaa zao ikawa hatari juu yao.

110. Watu wakifikwa na misukosuko hufanya yaliyokatazwa kwa balaa zinazowafika. Basi wanapewa bishara ya kusamehewa.

neema za Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye.

نِعْمَتَ اللَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١١٤﴾

115. Amekuharimishieni nyamafu tu (mzoga) na damu na nyama ya nguruwe na (mnyama) achinjwaye kwa jina lisilokuwa la Mwenyezi Mungu Lakini anayekosa budi (anayeshurutishwa) bila kuasi wala kuruka mipaka, basi (Mwenyezi Mungu atamsamehe); hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالدَّمَ وَلَحْمَ
الْخِنزِيرِ وَمَا أُهِلَّ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ
غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٥﴾

116. Wala msiseme, kwa sababu ya uwongo usemao ndimi zenu, "Hii ni halali na hii ni haramu," msije mkamzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wale wamzuliao uwongo Mwenyezi Mungu hawatafaulu.

وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ
هَٰذَا حَلَالٌ وَهَٰذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ
الْكَذِبَ ۚ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ
الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١١٦﴾

117. Ni starehe ndogo (tu hii hapa ya kiduniani); nao watapata adhabu iumizayo.

مَتَاعٌ قَلِيلٌ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١١٧﴾

118. Na Mayahudi tuliwaharimishia yale tuliyokuhadithia zamani. Na sisi hatukuwadhulumu, bali walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا مَا قَصَصْنَا
عَلَيْكَ مِن قَبْلُ ۖ وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَٰكِن كَانُوا
أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١١٨﴾

119. Kisha hakika Mola wako kwa wale waliofanya ubaya kwa ujinga, kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema; bila shaka Mola wako baada ya hayo ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu (kwao kama alivyo hivi kwa wenzi wao).

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ عَمِلُوا السُّوءَ بِجَهَالَةٍ
ثُمَّ تَابُوا مِن بَعْدِ ذَٰلِكَ وَأَصْلَحُوا إِنَّ رَبَّكَ
مِن بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٩﴾

---

115. Hapa imewekwa dhahiri ya kuwa ni unajisi na haramu kula mnyama anayechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali kwa ajili ya Shetani kama mnyama anayechinjiwa pepo au anayechinjiwa Shetani wa nyumba au Shetani wa kisima au Shetani wa mwaka au Shetani wa nchi au kwa ajili ya mashindano tu kama yaliyokuwa hapo zamani. Na miongoni mwa hayo ni mashindano ya vyama vya Maulidi na vyama vya ngoma na kwimba mfano wa nyimbo hizi:–

| | |
|---|---|
| Pili tasifu harufu | Nchi kutosikizana |
| Kwa mapande ya manofu | Kila unayemwona |
| Meongoka waongofu | Toba sitasema tena |
| Ngome ikipiga zumbe | Siraji hufazaika |

(HAYA NI MAJINA YA VIKAO)

| | |
|---|---|
| Huhisabu zao ng'ombe | Khamsini kutamka |
| Kulima kwataka jembe | Na mikono ya kunyoka |

Basi wanyama namna hawa wakichinjwa juwa najisi, haramu kuliwa. Na tazama Aya ya 3 ya *Suratul Maidah.*

Na zile nyama zilizotajwa kuwa ni haramu kuliwa kama hizo:– (a) Nyamafu (b) Damu (kama wanazokunywa wenye Pepo na kama wanavyofanya baadhi ya wakaazi wa Bara: humtoboa mnyama wakakinga damu wakanywa kisha wakamziba. (c) Nyama ya nguruwe. Basi nyama namna hizo ikiwa hapana budi kuzila kwa ajili ya njaa ya kutoa roho basi itakubalishwa kuliwa, Mwenyezi Mungu ana rehema kubwa juu ya viumbe vyake.

116. Kukata hukumu ya kuwa jambo hili Halali au Haramu kunahitaji ujuzi barabara; asijisemee tu mtu kuwa hili Halali, hili Haramu—asiseme ila awe na hoja ya kusema hayo.

118. Imebainishwa katika Aya ya 146 ya *Suratil An-Am* baadhi ya mambo waliyoharimishiwa Mayahudi.

120. Hakika Ibrahimu alikuwa Imamu (mfano mzuri wa wema wa kuigwa), mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina

إِنَّ إِبْرَٰهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِّلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ
يَكُ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾

121. (Alikuwa) mwenye kuzishukuru neema Zake (Mwenyezi Mungu zilizo juu yake), akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyoka.

شَاكِرًا لِّأَنْعُمِهِ ٱجْتَبَىٰهُ وَهَدَىٰهُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ
مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾

122. Na tukampa wema katika dunia; na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (pia).

وَءَاتَيْنَٰهُ فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَإِنَّهُ فِى ٱلْءَاخِرَةِ
لَمِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٢٢﴾

123. Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahimu (aliyekuwa) mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

ثُمَّ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ أَنِ ٱتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ
حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾

124. Hakika (adhabu ya kuvunja taadhima ya) Jumaamosi iliwekwa juu ya wale waliohitalifiana kwa ajili ya hiyo (Jumaamosi), na kwa yakini Mola wako atahukumu baina yao siku ya Kiama katika yale waliyokuwa wakihitalifiana.

إِنَّمَا جُعِلَ ٱلسَّبْتُ عَلَى ٱلَّذِينَ ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ
وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ فِيمَا
كَانُوا۟ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٢٤﴾

125. Waite (waite watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mauidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (siyo kwa kuwatukana wao au kutukana dini yao. Kwa njia hii huwezi kumvuta mtu) Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake, naye ndiye anayewajua walioongoka.

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ
ٱلْحَسَنَةِ وَجَٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ
هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ
بِٱلْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

126. Na mkilipiza, basi lipizeni sawa na vile mlivyoonewa. Na kama mkisubiri (msilipize) hakika huo ni ubora kwa hao wanaosubiri.

وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا۟ بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُم بِهِ
وَلَئِن صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ لِّلصَّٰبِرِينَ ﴿١٢٦﴾

127. Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu: Wala usihuzunike kwa ajili yao (kwani wanajipoteza wenyewe kwa khiari yao), wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila wanazozifanya.

وَٱصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلَّا بِٱللَّهِ وَلَا تَحْزَنْ
عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُ فِى ضَيْقٍ مِّمَّا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٧﴾

128. Kwa hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema.

إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوا۟ وَّٱلَّذِينَ هُم
مُّحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾ ع

124. Habari ya kuvunja Mayahudi taadhima ya Jumaamosi na adhabu iliyowapata imetajwa mahala pengi katika Qurani. Miongoni mwa mahala humo ni Aya ya 163 ya *Suratil Aaraf* mpaka aya ya 166.

125. Namna ya kuhingana ni hii. Maneno matamu humtoa nyoka pangoni, seuze yawe ni ya akili pia. Tumebainisha katika Aya ya 253 ya *Suratul Baqarah* na katika Aya ya 90 ya *Suratul An-am,* namna gani Mwenyezi Mungu alivyowafadhilisha hao Mitume waliokuwa kabla ya Nabii Muhammad.

126-127. Katika mazuri kabisa yaliyomo katika Qurani.